



Nishani ya usalama wa kambi (Camp safety)

Nishani hii ipo katika kundi la maburudisho na michezo (recreation), huwakilishwa kwa rangi ya kijani




By: Yusuph Mwasiposya

Usalama wa kambi

- Ni vema kufuatilia kanuni na sharia za serikali kuhusu uwashaji wa moto wa kambi mahali husika kwa sababu, katika sehemu nyingi ni marufuku kuwasha moto ya kambi pasipo ruhusa.
- Ruhusa hizo hupatikana kutoka kwenye mamlaka za zimamoto
- Wakati mwingine ruhusa inaweza kukataliwa kutokana na hali halisi ya mahali panapotakiwa kuwashwa moto, ikiwa kuna hatari ya moto kuwazidi wawashaji, mamlaka hii inaweza kuzuia kibali cha uwashaji moto mahali hapo
- Kuwasha moto pasipo ruhusa katika maeneo hayo kunaweza kumsababisha muwashaji kesi ya kijibu kwa mujibu wa sheria.

2

Usalama wa kambi

Unapokuwa kambini unapaswa kuhakikisha kuwa moto uliowashwa unapaswa kuwa katika uangalizi wakati wote kwa sababu:

- Usipoangaliwa unaweza ukazidi na kukushinda
- Unaweza kuwa hatari kwa watoto wanaocheza karibu na moto pasipo uangalizi
- Ni kinyume na sheria kuwasha moto pasipo na uangalizi makini

3

Sheria za usalama wa moto

- Weka moto mahali pasipo na nyasi au chochote cha kushika moto kirahisi na kuifanya usambae, inapendekezwa kuhakikishwa kuwa eneo liwe safi ndani ya mita 3 za kuzunguka eneo la moto
- Usiwashe moto karibu na matawi ya miti yanayoning'ina
- Washa moto bila kutumia vichochezi kama mafuta ya taa
- Kabla ya kuondoka eneo hilo, hakikisha eneo ni safi kabisa na moto umezima kabisa na kubaki majivu
- Usiwashe moto juu ya vitu viwezavyo kushika moto haraka na kuusambaza
- Hakikisha vifaa vya kuzimia moto haviko mbali nawe wakati wote moto unapokuwa unawake
- Usiondoe vijiti viwakavyo kutoka kwenye moto
- Kuwa mwangalifu kwa vipande vya moto vinavyoruka kutoka kwenye moto, na hakikisha unavizima haraka sana
- Funika miguu yako vizuri wakati wa kuota moto
- Usichome vitu vinavyoweza kuelea vikiwa na moto ili kuzuia kusambaa kwa moto. Mfano karatasi
- Usiwashe moto wakati wa upepo mkali ili kuzuia moto usije ukasambaa

4

Utunzaji wa chakula

- Ikiwa chakula kitapaswa kuliwa kikiwa cha moto basi sharti kitunzwe kwenye joto lenye nyuzijoto zisizopungua 60°C
- Ikiwa chakula kitapaswa kuliwa kikiwa cha baridi basi sharti kitunzwe kwenye joto lenye nyuzijoto zisizozidi 4°C
- Hii ni kwa sababu joto kati ya 4°C na 60°C ni hatari kwa chakula, maana hayo ni mazingira mazuri kwa bakteria wanaoharibu chakula kukua.
- Bacteria hawa wanaweza kusababisha chakula kuchacha, na chakula kilichochacha husababisha magonjwa

5

Namna ya kuzuia Wanyama wakali kuja katika kambi

- Osha vyombo vyote mara baada ya kumaliza kula
- Tunza chakula sehemu ambayo hawawezi kufika au ning'iniza chakula mahali ambapo Wanyama hawawzi kufika
- Usilete chakula hemani mahali pa kulala
- Weka vyombo vyako mahali pasafi na weka mahali ambapo Wanyama hawawezi kufika
- Choma moto mabaki ya chakula yasiyoweza kutumika tena

6

Usalama wa ujenzi wa choo

- Choo kiwe umbali wa mita 60 kutoka katika vyanzo vya maji.
- Choo lazima kiwe katika hali ya usiri
- Choo ni lazima kiwe na uwezo wa kubeba uzito wa kila mtu
- Lazima kuwe na vyoo tofauti kwa ajili ya jinsia zote
- Choo lazima kizingatie muda wa kukambika na idadi ya wanakambi ili kuepuka usumbufu wa kujenga choo kingine.
- Choo kinapaswa kiwe mbali na mahali pa kuandalia, kutunzia au kulia chakula.
- Choo hakipaswi kuwa karibu sana na mahali pa kulala, pia hakipaswi kuwa mbali sana na mahali pa kulala

7

Vifaa vya first aid kit

- Bandaji
- Gozi
- Dawa za kutuliza maumivu
- Tweezers (kwa ajili ya kuondoa chawa na viroboto)
- Dawa ya maunguzo.
- Dawa za kuchua.
- Dawa za vidonda.
- Mkasi.
- Gloves.
- Wembe n.k.

8

Usafi kambini

- Taja vitu vya kuzingatia wakati unafanya usafi kambini ambapo Hakuna maji yanayotembea
- Kuwa kambi hakumaanishi kuwa mchafu, ingawa usafi wa kambi si sawa na usafi wa nyumbani.
- Jenga bafu zuri na uliweke katika muelekeo mzuri na kuruhusu maji machafu kutoka nje ya bafu.
- Joto la maji linaweza kurekebisha kwa kuchanganya maji baridi na maji moto kidogo
- Usisafishe meno na kutema maji yake hovy, tumia sehemu maalumu
- Tumia njia ya usalama Zaidi kunawa mikono baada ya kutoka chooni.
- Usinywe maji yasiyotibiwa au kuchemshwa sawasawa

9

Namna ya kusafisha maji kambini

- Kuchemsha
- Njia hii hufanya maji kuwa salama kabisa
- Iodine
- Iodine huwekwa ndani ya maji kama kimiminika, chengachenga au kidonge.
- Njia hii huondoa vijidudu aina nyingi ingawa si vyote
- Baada ya kuweka iodine, tumia dawa nyingine ilikuondoa harufu ya iodine ndani ya maji.
- Chlorine
- Ni vema dawa hii ikatumika kwa dharura tu.
- Weka matone 2 katika lita 1 ya maji ikiwa ni maji angavu
- Acha kwa dakika 30 hadi 60.
- Baada ya hapo yafungue ili kuondoa harufu na ladha ya chlorine kutoka kwenye maji

10

Namna ya kusafisha maji kambini

- Filtering (kuchuja)
- Maji machafu huchujwa na kuingia katika chupa nyingine pasipo uchafu

11

Utunzaji wa kisu kambini

- Hakikisha kisu ni kikali wakati wote.
- Hakikisha kisu kinatunzwa katika ala yake wakati hakitumiki.
- Usiweke kisu karibu nawe kikiwa wazi
- Usitupe au kurusha kisu.
- Usichomeke kisu ardhini.
- Usigawe au kupokea kisu ukiwa unaangalia pembeni.

12

Sheria za matumizi ya shoka

1. Jifunze kutumia shoka kwa usahihi
2. Hakikisha Hakuna mtu aliye karibu na wewe wakati wa kukata kuni. Kukwa makini maana shoka laweza kuchomoka 2Falme 6:5
3. Unapochanja kuni hakikisha lile gogo linalochanjwa limeyekwa juu ya gogo lingine ili kukurahisishia kazi
4. Shusha shoka lako katika eneo ambalo halitasababisha gogo ulilolikanyaga kubadilisha mkao, maana hii inaweza kukusababisha majeraha. Kuwa makini
5. Shika shoka lako kwa mikono yote miwili
6. Usiweke miguu yako sehemu moja wakati wa kupasua kuni

13

Sheria za matumizi ya msumeno

1. Usichote kitu kwa kutumia msumeno, msumeno ni kwa ajil ya kukatia tu.
2. Weka vidole mbali na makali au meno ya msumeno.
3. Anza kukata kutoka katika kona ili msumeno usiruke toka sehemu unayokata.
4. Tunza msumeno katika sehemu sahihi wakati unapokuwa hautumiki.
5. Kuwa makini na msumeno mzima wakati wa kukata.
6. Usikate kitu kinachoshikilia kitu kingine.

14

Sheria za matumizi ya kibiriti

1. Yeyote anayetumia kibiriti ni vema asimamiwe (ikiwa ni mtoto)
2. Weka kibiriti mbali na watoto.
3. Usiwashe kibiriti karibu na mwili wako.
4. Tunza vema kibiriti ikiwa hakitumiki.



15

Aina za nishati kambini

- Propane
 - Hii ndio nishati inayotumika sana kambini.
 - Hakikisha unafunga vema mtungi wako mara baada ya kumaliza kupika.
 - Wakati wa kuwasha jiko, hakikisha kibiriti chako kimewashwa kabisa kabla ya kufungua gesi yako.
 - Ukifungua gesi kable ya kuwasha kibiriti, unaweza ukasababisha mlipuko.
 - Kama jiko halijawaka, subiri kwa muda kidogo ili gesi ipotee hewani ndipo ujaribu kuwasha tena

16

Aina za nishati kambini

- Pombe
 - Nishati hii hutumika sana kwa safari za backpacking.
 - Kuwa makini kwa sababu moto wa nishati hii mara nyingine kuwa hauonekani hasa wakaati wa jua.
 - Watafutanjia wanaweza kwenda kuuwasha upya kwa kudhani kuwa umezima.

17

Rejea

- "https://en.wikibooks.org/w/index.php?title=Adventist_Youth_Honors_Answer_Book/Recreation/Camp_Safety&oldid=3251028"



18